**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**ILIYOKAA MOROGORO**

**SHAURI LA MAREJEO NA. 07 LA 2019**

**KATI YA**

**21ST CENTURY TEXTILES LIMITED.............................MLETA MAOMBI**

**NA**

**ELVIS PROSPER KOOLA...........................................MJIBU MAOMBI**

**HUKUMU**

**Tarehe ya Amri Ya Mwisho: 25/05/2021**
**Tarehe ya Hukumu: 04/06/2021**

**A.E MWIPOPO, J.**

Shauri hili la marejeo limefunguliwa dhidi ya Uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi katika Mgogoro wa Kazi Na. RF/CMA/MOR/136/2017. Mleta Maombi ambaye ni 21st Century Textiles Limited anaomba Mahakama itoe amri zifuatazo:-

1. Kwamba Mahakama hii iitishe rekodi za Tume ya Usuluhishi na Uamuzi katika mgogoro wa kazi Na. RF/CMA/MOR/136/2017 kati ya wadaawa waliomo katika shauri hili ambapo tuzo ya Tume ilitolewa na Mhe. Hiraly, Muamuzi, tarehe 14 Disemba, 2018, tuzo hiyo irekebishwe na ifutwe kwa kiasi kwamba amri ya kulipa jumla ya Tshs. 1,797,148/= ikiwa ni mapunjo ya muda wa nusu saa ya mapumziko ya mchana dhidi ya Mleta Maombi na iwekwe pembeni (set aside).

2. Mahakama hii ikipendezwa itoe nafuu au amri nyingine yoyote kwa Mleta Maombi kama itakavyoona inafaa na ya haki (just) kuitoa.

Shauri hili limeungwa mkonon na kiapo cha Hassan Dewji ambaye ni Ofisa Mkuu wa Mleta Maombi. Kiapo hicho katika aya ya 4 kimetaja masuala mawili ya kisheria (legal issues) ya kuangaliwa yanayotokana na ushahidi muhimu. Masuala hayo ni:-

i. Iwapo Muamuzi alikuwa sahihi kuamua kumpa madai ya nusu saa ya muda wa mapumziko ya chakula cha mchana uliopunguzwa, kinyume cha kifungu cha 23(3) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, Sheria Na. 6 ya 2004.

ii. Iwapo kumpatia madai ya nusu saa ya muda wa chakula yaliyopunjwa yanakumbatia ubaguzi miongoni mwa wafanyakazi wa Mleta Maombi.

Historia fupi ya shauri hili ni kwamba Mjibu Maombi aitwaye Elvis Prosper Koola aliajiriwa na Mleta Maombi mnamo tarehe 1 Julai, 2012 katika nafasi ya Fundi Umeme. Aliachishwa kazi kwa sababu za kinidhamu tarehe 30 Juni, 2017. Mjibu Maombi hakuridhika na uamuzi wa Mleta Maombi na akawasilisha mbele ya Tume mgogoro wa kazi kuwa aliachishwa kazi isivyo halali. Tume ilitoa uamuzi wake tarehe 14 Disemba, 2018 na kuona kuwa uachishwaji kazi wa Mjibu Maombi ulikuwa halali na wa haki ila iliona kuwa Mjibu Maombi alipunjwa muda wake wa mapumziko ya mchana na hivyo kuamuru alipwe Tshs. 1,797,148/= kama

malipo ya kukatwa nusu saa ya chakula na Tshs. 40,570/= ikiwa ni makato ya siku 4 katika mshahara wake. Mleta Maombi hakuridhika na tuzo ya malipo ya madai ya makato ya nusu saa ya chakula iliyotolewa na Tume na akawasilisha shauri hili la marejeo hapa Mahakamani.

Akiwasilisha hoja zake kuunga mkono marejeo haya, Wakili wa Mleta Maombi aitwaye Bw. Adam Mwambene alieleza kuwa wanaomba Mahakama hii kupitia uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi na kuutengua kwa kuwa malipo yaliyotolewa hayakuwa halali. Malipo hayo ni ya chakula cha mchana ambayo yapo kinyume na sheria. Alieleza kuwa Mleta maombi anayo sababu moja tu ya kuleta marejeo haya ambayo ni endapo mwamuzi alikuwa sahihi kuamua kutoa malipo ya muda wa nusu saa uliotolewa kwa ajili ya chakula cha mchana ambayo ni kinyume cha Kifungu cha 23(3) ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, sheria na. 06 ya 2004. Kifungu cha 23(1) cha sheria kinaeleza kuwa mwajiri anatakiwa kumpa mwajiriwa aliyefanya kazi mfululizo kwa zaidi ya masaa 5 angalau dakika 60 za mapumziko. Kifungu kidogo cha (2) kinasema kuwa mwajiri anaweza kumwambia mwajiriwa kufanya kazi wakati wa mapumziko ikiwa kazi haiwezi kuachwa bila mtu au haiwezi kufanywa na mwajiriwa mwingine. Aidha kifungu kidogo cha (3) kinaeleza kuwa mwajiri hatatakiwa kumlipa mwajiriwa kwa kipindi cha mapumziko isipokuwa pale ambapo mwajiriwa atatakiwa kufanya kazi au awapo kwa ajili ya kazi wakati wa mapumziko. Katika shauri hili mjibu maombi alikuwa anapata

mapumziko ya mchana kama wafanyakazi wengine katika kipindi chote cha ajira yake.

Wakili alieleza kwa Muamuzi katika uamuzi wake aliona kuwa mkataba wa mjibu maombi ulitoa muda wa nusu saa tu kwa ajili ya chakula cha mchana. Na sheria inasema kuwa mwajiri halazimiki kumlipa mwajiriwa kwa ajili ya muda wa chakula cha mchana. Hivyo Muamuzi alikosea.

Wakili aliendelea kueleza kuwa madai ya makato ya muda wa nusu saa kwa ajili ya chakula cha mchana yaliwasilishwa mbele ya Tume yakiwa nje ya muda. Muamuzi hana Mamlaka ya kushughulikia na kuayatolea Uamuzi madai yaliyotolewa nje ya muda. Mjibu maombi alianza kazi tarehe 27 Machi, 2012 na alifanya kazi hadi tarehe 30 Juni, 2017. Makato ambayo Muamuzi alimpatia yalihesabiwa kuanzia alipoanza kazi hadi ajira yake ilipositishwa. Katika shauri hili hakukuwahi kuwa na maombi ya kuongezwa muda wa kuwasilisha madai ya kupunjwa muda wa mapumziko. Hivyo madai hayo yanapinga kanuni ya 10(2) ya Tangazo la Serikali Na. 67 la 2007 ambayo inataka madai ambayo sio ya kuachishwa kazi yanatakiwa yawasilishwe ndani ya siku 60 tokea tarehe ya madai hayo kuanza au mgogoro wa madai hayo kuanza. Muamuzi alitoa madai hayo yakiwa yamepitwa na wakati kwa miaka 5. Mahakama hii imeeleza kuwa ukomo wa muda ukipuuzwa unapelekea Tume ikose Mamlaka kama ilivyoelezwa katika kesi ya **Muccobs dhidi ya Christian Maondo,**

**marejeo na. 21 ya 2003** LCCD 2015 part 1 katika ukurasa 194. Mahakama iliona kuwa suala la ukomo wa muda ni la msingi linaloenda katika Mamlaka ya Mahakama na linahakikisha kuwa Mdaawa haji vile na pale ambapo atajisikia kufanya hivyo.

Alieleza kuwa katika shauri la **Glory Moshi dhidi ya limesina, maombi na. 41 ya 2014,** Mahakama Kuu, Divisheni ya Kazi, LCCD 2014 part 1 ukurasa 249 ilieleza kuwa shauri ambalo limewasilishwa nje ya muda linatakiwa litupiliwe mbali (dismiss) na shauri lililotupiliwa mbali haliwezi kufufuliwa. Kushindwa kwa suala la ukomo wa muda kuzingatiwa na Tume kama tulivyoona katika kesi zote mbili kunafanya shauri husika liwe batili. Kwa kuwa Muamuzi hakuzingatia matakwa ya sheria na uhalali wa maombi yaliyowasilishwa mbele yake ione kuwa maombi hayo yalikuwa batili. Hivyo Mleta Maombi anaomba Mahakama itengue Tuzo hiyo kwa kiwango cha malipo yaliyotolewa na Muamuzi.

Akijibu Mawasilisho ya Mleta Maombi, Bw. Hamisi Salum, Mwakilishi Binafsi wa Mjibu Maombi, alieleza kuwa wakati wa usikilizwaji wa shauri Tume iliona kuwa Mjibu Maombi anastahili kulipwa mafao ya muda wa mapumziko yaliyokuwa yanakatwa pamoja na makato ya mshahara wake. Malipo ya makato ya mshahara ya Mleta Maombi hayajapingwa. Aya ya 7 ya mkataba wa ajira wa Mjibu Maombi inasema kuwa atapewa muda wa nusu saa kwa ajili ya mapumziko. Utaratibu wa mwajiri ulikuwa kwamba waajiriwa walikuwa wanakatwa kiasi cha fedha kwa ajili ya chakula na

kiasi hicho wanarudishiwa baada ya kumaliza mikataba yao. Haki hiyo ya mapumziko haikusema kuwa watakatwa mishahara yao. Na hiyo hela anayokatwa mwajiriwa hurudishwa akiacha au kuachishwa kazi. Kwa sababu hiyo, haikuwa sahihi kudai malipo hayo kabla mwajiriwa hajaacha au kuachishwa kazi. Mgogoro huo ulianza baada ya kuachishwa kazi. Madai haya yapo ndani ya muda, mgogoro ulianza baada ya mwajiriwa kuachishwa kazi na mwajiri kukaa kimya bila kutoa malipo yoyote. Hivyo, Mjibu Maombi anaona kuwa tuzo iliyotolewa na Tume ya Makato ya chakula katika mshahara wa mjibu maombi ilikuwa ni sahihi. Mleta maombi alikiuka masharti ya mkataba wa mjibu maombi.

Katika mawasilisho ya nyongeza (rejoinder submission) ya wakili wa Mleta Maombi alieleza kuwa Kifungu cha 7.5 cha mkataba hakisemi kuwa mjibu maombi atakatwa kwa muda atakaotumia wakati wa mapumziko. Mkataba ulitekeleza matakwa ya sheria ya kumpa mjibu maombi muda wa mapumziko.

Kutokana na mawasilisho ya pande zote mbili, ni wazi kuwa Mleta Maombi amewasilisha marejeo haya kupinga tuzo ya malipo ya makato ya muda wa mapumziko ya mchana. Na sababu za kupinga tuzo hizo ni mbili, kwanza tuzo hiyo ipo kinyume cha sheria na pili Mjibu Maombi hakuwa amewasilisha madai hayo ya kulipwa makato ya muda wa chakula cha mchana kwa wakati mbele ya Tume.

Katika sababu ya kwanza ya Marejeo Mleta Maombi alieleza kuwa Mjibu Maombi alikuwa anapata mapumziko ya mchana kama wafanyakazi wengine katika kipindi chote cha ajira yake. Na kuwa kifungu cha cha 23(3) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kinaeleza kuwa mwajiri hatatakiwa kumlipa mwajiriwa kwa kipindi cha mapumziko isipokuwa pale ambapo mwajiriwa atatakiwa kufanya kazi au awapo kwa ajili ya kazi wakati wa mapumziko. Kwa upande wa Mjibu Maombi yeye alieleza kuwa alikuwa akikatwa nusu saa ya chakula katika masaa 4 ya ziada badala ya muda huo kutolewa katika masaa 8 ya kazi ya kawaida. Kitendo cha kupunguza nusu saa katika masaa ya ziada maana yake malipo yake ya muda wa ziada wakati wakati masaa hayo alikuwa anayafanyia kazi.

Nimeangalia kifungu cha 23 cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ambacho kwa ujumla wake kinaongelea mapumziko wakati wa kazi. Kifungu hicho kinaeleza kwamba, nanukuu:-

> *"23.-(1) Kwa kuzingatia Sehemu hii, mwajiri anatakiwa kumpa mfanyakazi ambaye amefanya kazi mfululizo kwa zaidi ya saa tano mapumziko ya angalau dakika sitini.*
>
> *(2) Mwajiri anaweza kumtaka mfanyakazi kufanya kazi wakati wa mapumziko ikiwa tu kama kazi haiwezi kufanywa na mfanyakazi mwingine.*
>
> *(3) Mwajiri hatakiwi kuwajibika kumlipa mfanyakazi katika kipindi cha mapumuziko isipokuwa kama mfanyakazi anatakiwa kufanya kazi au kuwepo kwa ajili ya kazi wakati wa mapumziko."*

Kama alivyoeleza wakili wa Mleta Maombi sheria tajwa hapo juu inaeleza kuwa mwajiri hatakiwi kuwajibika kumlipa mfanyakazi katika

kipindi cha mapumuziko isipokuwa kama mfanyakazi anatakiwa kufanya kazi au kuwepo kwa ajili ya kazi wakati wa mapumziko. Hata hivyo, hoja ya Mjibu Maombi ni kuwa muda wa nusu saa ya mapumziko ulikuwa unakatwa katika muda wa masaa ya ziada badala ya kukatwa katika muda wa kawaida wa masaa ya kazi hivyo kupelekea kupungua kwa malipo ya masaa yake ya ziada. Aidha, katika fomu ya Tume Na. 1, Mjibu Maombi alitolea ufafanuzi wa mapunjo hayo ambayo jumla yake inaonekana ni shilingi 1,353,866.02. Pamoja na kuwa kifungu cha 23(3) cha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini kimeeleza kuwa mwajiri hatakiwi kuwajibika kumlipa mfanyakazi katika kipindi cha mapumuziko isipokuwa kama mfanyakazi anatakiwa kufanya kazi au kuwepo kwa ajili ya kazi wakati wa mapumziko, lakini Mjibu Maombi alionesha kuwa muda huo ulikatwa katika malipo yake ya saa za ziada. Hii inamaanisha kuwa malipo yake ya saa za ziada yalikuwa pungufu. Na Mleta Maombi hakupinga hoja hii ya Mjibu Maombi kwa ushahidi. Kwa sababu hiyo, ninaona kuwa madai ya Mjibu Maombi kuhusu makato yake ya muda wa nusu saa ya mapumziko yalikuwa yamethibitishwa na hayapo kinyume cha sheria kama ilivyoamuliwa na Tume.

Mleta Maombi alieleza kuwa madai ya makato ya muda wa nusu saa kwa ajili ya chakula cha mchana yaliwasilishwa mbele ya Tume yakiwa nje ya muda hivyo Muamuzi hakuwa na mamlaka ya kushughulikia na kuyatolea Uamuzi. Makato ambayo Muamuzi alimpatia yalihesabiwa

kuanzia alipoanza kazi hadi ajira yake ilipositishwa. Na katika mgogoro uliokuwa mbele ya Tume Mjibu Maombi hakuwahi kuomba kuongezwa muda wa kuwasilisha madai ya kupunjwa malipo ya muda wa mapumziko. Hivyo madai hayo yanapinga kanuni ya 10(2) ya Tangazo la Serikali Na. 67 la 2007 kwa kuwa yaliwasilishwa nje ya siku 60 tokea tarehe ya madai hayo kuanza au mgogoro wa madai hayo kuanza. Kwa upande wa Mjibu Maombi alieleza kuwa madai hayo yaliwasilishwa mbele ya Tume ndani ya muda kwa kuwa mgogoro ulianza baada ya mwajiriwa kuachishwa kazi na mwajiri kukaa kimya bila kutoa malipo yoyote.

Mjibu Maombi aliomba alipwe madai ya makato ya muda wa nusu saa ya mapumziko tokea alipoanza kazi hadi alipoachishwa na Tume ilimpatia tuzo hiyo. Katika ushahidi wake Mjibu Maombi alieleza kuwa alikuwa anakatwa masaa hayo kuanzia anaanza kazi hadi tarehe aliyoachishwa kazi. Hii ina maana kuwa katika kipindi chote cha mkataba wake wa kufanya kazi alikuwa akipunjwa malipo ya muda huo wa mapumziko. Ni maoni yangu kuwa Mjibu Maombi alikuwa akipunjwa malipo ya saa za ziada hadi tarehe ya kuachishwa kazi hivyo kulikuwa na mwendelezo wa kunyimwa haki yake hadi tarehe hiyo aliyoachishwa kazi. Hivyo, mgogoro ulikuwa ukiendelea kutokea kila linapokuja suala la malipo yake ya saa za ziada, malipo yaliyokuwa yakitolewa pamoja na mshahara kama karatasi ya mshahara (salary slip) inavyoonesha. Hivyo, ni maoni

yangu kuwa mgogoro huo uliwasilishwa ndani ya muda na Tume ilikuwa na mamlaka ya kuusikiliza na kuutolea uamuzi.

Hata hivyo, nimeona kuwa Mleta Maombi aliambatisha mchanganuo wa madai yake ya makato ya fedha hiyo ya muda wa mapumziko katika fomu Na. 1 ya Tume. Na madai hayo yanaonesha kuwa anadai shilingi 1,353,866.02. Lakini Tume iliamuru alipwe shilingi 1,797,148/= ambazo alikuwa amezitaja katika maelezo ya awali ambayo hayakuwa yametolewa mchanganuo. Naona kuwa Tume ilikosea kuona kuwa tuzo aliyostahili ni shilingi 1,797,148/= wakati katika fomu yake ya kuwasilisha mgogoro mbele ya Tume aliambatisha kielelezo kinachotoa kiasi kingine kilicho na mchanganuo.

Hivyo, naifuta (set aside) tuzo ya shilingi 1,797,148/= iliyotolewa na Tume. Mleta Maombi atamlipa Mjibu Maombi shilingi 1,353,866.02/= ikiwa ni makato ya malipo ya muda wa mapumziko. Malipo haya ni nyongeza ya shilingi 40,570/= ambazo Mleta Maombi anatakiwa kumlipa Mjibu Maombi kutokana na makato ya mshahara ya siku 4. Na hivyo jumla ya fedha yote ambayo Mleta Maombi atamlipa Mjibu Maombi ni shilingi 1,394,436.02/=. Kwa kuwa hili ni shauri la kazi, kila upande utajigharamia gharama zake za kuendesha shauri hili.

**A. E. MWIPOPO**
**JAJI**
**04/06/2021**